

UQAB

Jarida la

TAARIFA KWA VYOMBO

VYYA HARABI

Amerika Inarefusha
Mzozo nchini Sudan
ili Kuwalazimisha Raia
Kukubali Utawala wa
Kijeshi

HABARI NA MAONI

Ni Nani

Atakayekomesha
Mauaji ya Waislamu na
Ubomoaji wa Misikiti
Nchini Ethiopia

MATOLEO

Jua kuhusu mwokozi
wa maisha, Hizb ut
Tahrir, ulinganizi wao
kwa Uislamu, Khilafah
na njia yake

JIBU LA SWALI

Kafara ya
Kuvunja Kiapo
(Kafarat ul-Yameen)

Eid
Al-Adha
MUBARAK

Salamu kutoka kwa Amiri wa Hizb ut Tahrir, Mwanachuoni Mkubwa

Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah

Kwa Wanaozuru Kurasa zake Mtandaoni kwa Mnasaba wa Idd ul-Adha Al-Mubaraka ya Mwaka 1444 H sawia na 2023 M

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu na rehma na amani zimshukie Mtume wa Mwenyezi Mungu, na jamaa zake na maswahaba zake na waliomfuata.

Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar, La Ilaha Ila Allah, Allahu Akbar, Allahu Akbar, Wa lillah Alhamd

Kwa Ummah zima wa Kiislamu kwa jumla... Umma bora ulioletwa kwa wanadamu ambao unaamrisha Ma'roof (mema) na unakataza Munkar (maovu) na unamuamini Mwenyezi Mungu Al-Aziz Al-Hakim...

Kwa wabebaji dawa haswa... Mwenyezi Mungu alete ushindi kupitia mikono yao, na Mwenyezi Mungu awanusuru kusimamisha dola ya Kiislamu, Khilafah Rashida kwa njia ya Utume...

Kwa wageni watukufu wa kurasa za mtandaoni, wanaotafuta kheri ambazo zinabeba, wakifanya bidii kutafuta haki na kuwanusuru watu wake.

Kwao wote,

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Ninakupongezeni kwa mnasaba wa Idd ul-Adha iliyobarikiwa...na ninamuomba Mwenyezi Mungu Al-Qawi Al-Aziz kwamba Idd hii iwe ni ufunguo wa kheri na baraka kwa Waislamu wote.

Ndugu na dada wapendwa, nawasalimu na kuwaombeeni dua ya kheri kwenu, nikimuomba Mwenyezi Mungu Al-Qawi Al-Aziz awaondolee Waislamu wote dhiki na janga, na kwamba mwezi huu mtukufu uwe ndio mwezi mtukufu wa mwisho kuwashukia Waislamu huku kukiwa hakuna Dola inayoleta izza kwa Uislamu na watu wake, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Muweza.

Mwenyezi Mungu azikubalie ibada zenu na akufanyeni miongoni mwa wale aliowasifu Mwenyezi Mungu (swt) katika aya hii:

رَجَالٌ لَا تُلْهِهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ يَخَافُونَ يَوْمًا تَتَقَلَّبُ فِيهِ الْقُلُوبُ وَالْأَبْصَارُ * لِيَجْزِيَ اللَّهُ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَيَزِيدَهُمْ مِنْ فَضْلِهِ [وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ]

“Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kushika Sala, na kutoa Zaka. Wanaikhofu Siku ambayo nyoyo na macho yatageuka. * Ili Mwenyezi Mungu awalipe bora ya waliyo yatenda, na awazidishie katika fadhila zake. Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.” [An-Nur: 37-38]

Ndugu Yenu,

Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah

10 Dhu al-Hijjah 1444 H

Amiri wa Hizb ut Tahrir

Sawia na 28 Juni 2023 M

Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

Amerika Inarefusha Mzozo nchini Sudan ili Kuwalazimisha Raia Kukubali Utawala wa Kijeshi

Marekani ilizindua kile ilichokiita jukwaa la Kuchunguza Mzozo wa Sudan. Mnamo tarehe 9 Juni 2023, afisi ya msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilitoa taarifa kuhusu suala hili, "Jukwaa la Kuchunguza Mzozo wa Sudan linathibitisha dhamira ya Marekani ya uwazi tunapofanya kazi na washirika ili kukomesha mzozo wa kijeshi nchini Sudan; kushughulikia ukiukaji na unyanyasaji wa haki za binadamu; na kuhakikisha ufikiaji wa haraka, salama, na usiozuiliwa wa msaada wa kibinadamu kwa mashirika yanayotoa usaidizi wa kuokoa maisha kwa wale walio hatarini zaidi na wale waliohamishwa kutokana na mapigano. Marekani haiyumbishwi katika kuunga mkono kwetu matakwa ya kidemokrasia ya watu wa Sudan na matakwa yao ya uhuru, amani na haki."

Imefahamika kwa kila mfuatiliaji wa siasa za Sudan kwamba Marekani ndiyo iliyowaagiza vibaraka wake, Burhan na Hemeti, kuchochea vita hivi vinavyoendelea nchini Sudan ili kuhujumu Azimio la Katiba linaloweka jeshi chini ya mamlaka ya kiraia, ambayo ina maana halisi ya uhamisho wa madaraka kutoka mikononi mwa wanajeshi wa Marekani kwenda kwa raia wa Uingereza ambao wanasimamia vita hivi kwa njia ambayo inazuia upande wowote kupata ushindi wa uhakika, kurefusha muda wa vita na kusukuma vyama vya kisiasa, hasa raia, katika hali ya kukata tamaa na hatimaye kukubali masharti yake, huku nguvu halisi ikibakia mikononi mwa wanajeshi wake. Taarifa hii iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani haiachi nafasi ya shaka kuhusu usimamizi wa Marekani wa mzozo huu, licha ya madai yake kwamba inajaribu kuumaliza, kama ilivyoielezwa katika taarifa hiyo ya kupotosha. Uhalisia unagongana na wanachosema, na kurudiwa kwa usitishaji mapigano ambao pande zote mbili haziuzingatii kuthibitisha uwongo na udanganyifu wa Marekani.

Ama ajabu kubwa kuliko maajabu yote kama msemu unavyosema, "msiba mbaya zaidi unakufanya ucheke" ni kile kilichosemwa katika taarifa kwamba Marekani inaunga mkono matarajio ya watu wa Sudan ya uhuru, amani na haki, wakati huo huo ikidumisha mshiko wake kwa Sudan kupitia jeshi! Inajulikana vyema kuwa Marekani inaunga mkono tu tawala za kidikteta na kijeshi katika nchi za Kiislamu zinazotawala watu wao kwa chuma na moto.

Sudan ni ardhi ya Kiislamu, na haitakombolewa kutoka kwa Marekani na watu wake, au kutoka kwa Uingereza na wafuasi wake, isipokuwa kwa kusimamisha dola iliyojengwa juu ya msingi wa Aqidah tukufu ya Uislamu, Aqidah ya Ummah wa Kiislamu, Khilafah Rashida kwa njia ya Utume inayoziunganisha nchi za Waislamu, kukata mikia ya makafiri na wafuasi wao, na kurudisha izza, adhama, na kheri ya Umma huu.

وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هُوَ قُلْ عَسَىٰ أَنْ يَكُونَ قَرِيبًا

“na watasema: Lini hayo? Sema: A'saa yakawa karibu!” [Al-Isra:51]

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Sudan**

HABARI NA MAONI

Ni Nani Atakayekomesha Mauaji ya Waislamu na Ubomoaji wa Misikiti Nchini Ethiopia

Habari:

Mnamo tarehe 2 Juni, kufuatia swala za Ijumaa, Waislamu 3 waliuawa na vikosi vya usalama vya Ethiopia nje ya Msikiti Mkuu, Msikiti wa Anwar jijini Addis Ababa, mji mkuu wa Ethiopia wakati wa maandamano ya amani ya kupinga uvunjaji wa mamlaka wa misikiti kadhaa nje ya mji na mipango kuvunja mengine zaidi. Polisi walitumia gesi ya kutoa machozi na kuwafyatulia risasi waumini ili kuutawanya umati uliokusanyika nje ya msikiti huo. Wiki iliyotangulia, Waislamu 2 waliuawa na makumi ya wengine kujeruhiwa na vikosi vya usalama katika eneo moja wakati wa maandamano mengine, huku Waislamu 114 pia wakiripotiwa kukamatwa. Baadhi waliripoti kuwa magari ya kubebea wagonjwa hayakuweza kuwafikia waliojeruhiwa kutokana na vikosi kuuzingira msikiti huo.

Maoni:

Katika miezi ya hivi karibuni, takriban misikiti 19 imebomolewa na mamlaka nchini Ethiopia kama sehemu ya mradi wenye utata wa kupanga miji unaohusisha ujumuishaji wa manispaa kadhaa katika eneo la Oromia nje ya mji mkuu na ujenzi wa mji mpya wa Shaggar ambao serikali inadai kuwa utaboresha uchumi na kuipamba Addis Ababa kama eneo la utalii wa mijini. Uamuzi wa serikali wa kubomoa zaidi ya misikiti 30 katika Mji mpya wa Shaggar umeibua hasira kubwa miongoni mwa Waislamu nchini humo ambao wamepanga maandamano mbalimbali kupinga hatua hiyo. Baraza Kuu la Shirikisho la Masuala ya Kiislamu la Ethiopia lilituma barua kwa Waziri Mkuu Abiy Ahmed kutaka kusitishwa kwa ubomoaji huo lakini iliangukia masikio ya uziwi. Mradi huo pia unahusisha uharibifu wa nyumba na biashara, ambao unaripotiwa kuwaacha maelfu bila makaazi.

Mnamo Aprili 2022, zaidi ya Waislamu 20 waliuawa na zaidi ya 150 kujeruhiwa katika shambulizi katika makaburi ya Sheikh Elias katika mji wa Gondar kaskazini mwa Ethiopia wakati wa mazishi ya mzee mmoja Muislamu. Tukio hilo pia lilishuhudia uporaji wa mali za Waislamu. Wahalifu hao walikuwa Wakristo wenye msimamo mkali. Mnamo mwaka wa 2019, misikiti mingi ilishambuliwa katika mji wa Mota huko Amhara katika wimbi la vurugu dhidi ya Waislamu.

Ethiopia au Habasha kama ilivyokuwa ikijulikana hapo zamani wakati mmoja ilikuwa ni hifadhi kwa Waislamu waliokuwa wakitafuta ulinzi dhidi ya mateso wakati wa Mtume (saw); ihifadhi moja ya misikiti mikongwe zaidi barani Afrika - Msikiti wa Al Nejashi; ina historia tajiri ya Uislamu ambayo inaenea kwa karne nyingi; na ina idadi

ya Waislamu zaidi ya milioni 25 - zaidi ya theluthi moja ya wakaazi. Lakini leo Waislamu wanauawa na maeneo ya kidini ya Kiislamu yanaharibiwa katika ardhi hii pasi na serikali, uongozi, mtawala aliye na utashi wa kisiasa kukomesha dhulma hii, ingawa Mtume (saw) amesema:

“كُتِلَ الْمُؤْمِنُ أَكْظَمُ عِنْدَ اللَّهِ مِنْ زَوَالِ الدُّنْيَا” **Kumuua muumini ni jambo kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko kuondoka dunia nzima.**” Hatutarajii chochote kutoka kwa serikali za Magharibi na UN isipokuwa maneno matupu ya kulaani. Hatutarajii chochote kutoka kwa tawala za sasa na watawala wa ulimwengu wa Kiislamu ambao wamethibitisha mara kwa mara kwamba hawana uchungaji wa kweli kwa utukufu wa damu ya Kiislamu au Uislamu.

Leo hii, haki za Waislamu nchini Ethiopia zinakanyagwa kama vile zinavyokanyagwa nchini India, Myanmar, Ufaransa na katika nchi nyenginezo duniani bila uongozi wa dhati wa Kiislamu wa kuwalinda. Hali hii haikuwa hivyo kila wakati. Wakati Waislamu nchini Uhispania, Palestina, India na kwengineko walipokuwa wakiteswa huko nyuma, Khilafah iliingilia kati kulinda damu zao na kuwakomboa kutoka kwa madhalimu wao. Ni dola hii pekee ndiyo yenye utashi wa kisiasa na uwezo wa kuwalinda Waislamu, popote wanapoishi, kutokana na madhara na mateso, kwani Mtume (saw) amesema:

“وَإِنَّمَا الْإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتِلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيَنْقَى بِهِ” **Hakika Imam ni ngao, watu hupigana nyuma yake na huhijami kwake.**” Hata hivyo, tangu kuvunjwa kwa Khilafah mnamo 3 Machi 1924, Waislamu kote duniani wamekuwa kama mayatima, waliotelekezwa, bila ya mlezi au mlinzi.

Baada ya kusimamishwa tena Khilafah kwa njia ya Utume, dola hii itataka kuziunganisha ardhi za Waislamu, rasilimali zao, mali zao na jeshi ili kujenga nguvu kubwa ambayo itatia hofu katika nyoyo za wale wanaosubutu kuwadhuru Waislamu, au kushambulia Dini yao au maeneo ya kidini. Itakuwa na nguvu kubwa za kisiasa, kiuchumi, kimkakati na kijeshi na kujiinua na kuonyesha kwa vitendo badala ya maneno matupu dori yake kama mlezi na ngao ya Waislamu na Uislamu. Hivyo tunawalingania kaka na dada zetu nchini Ethiopia na kote duniani kufanya kazi na Hizb ut Tahrir kusimamisha kwa dharura Khilafah ambayo itatangaza pambazuko jipya la usalama na ulinzi kwa Ummah huu.

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

**Dkt. Nazreen Nawwaz
Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika
Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Jua kuhusu mwokozi wa maisha, Hizb ut Tahrir, ulinganizi wao kwa Uislamu, Khilafah na njia yake



Mnamo tarehe 10 Mei 2023, baadhi ya majukwaa ya habari yakiwemo ya maandishi na televisheni yaliripoti kuhusu kuzuiliwa kwa hadi Waislamu 16 katika miji miwili - Bhopal na Hyderabad. Madai hayo ya kashfa yaliishambulia Hizb ut Tahrir kama shirika la 'Kigaidi' linalokusudia kufanya 'Jihad' dhidi ya India. Maregeleo yaliyotolewa kwa vyanzo 'visivyojulikana' kwa mashirika tofauti tofauti ya kijasusi (serikali na muungano) ikiwemo baadhi ya mashirika ya 'kigeni'. Umiliki wa machapisho ya vitabu vya Hizb ut Tahrir kwa wale waliowekwa kizuizini ulifanywa kuwa ndio msingi wa madai hayo. Tangu wakati huo riwaya tofauti za madai hayo zimekuwa zikienea mtandaoni, ikiwa ni pamoja na kuwahusisha Waislamu 16 waliokamatwa na kesi inayoendelea ya wanachama wa Hizb ut Tahrir katika jimbo la Tamil Nadu. Hata majukwaa mashuhuri ya habari kama vile 'India Today' au 'Economic Times of India' hayakuweza kuzingatia kanuni msingi za maadili, ambazo huchapishwa kwenye tovuti zao wenyewe, na kuvuta kwa urahisi 'simulizi' walizopewa bila kuchunguza ukweli wa kimsingi kuhusu Hizb ut Tahrir! Hivyo huu hapa ni utangulizi mfupi kuhusu Khilafah na Hizb ut Tahrir. Hizb ut Tahrir (Chama cha Ukombozi) ni chama cha kisiasa kinachofanya kazi ya kusimamisha tena Khilafah, mfumo wa utawala wa Kiislamu, katika ulimwengu wa Kiislamu kwa kuiga mfano wa Mtume (saw) kama njia yake.

Kuhusu Khilafah: Mfumo wa utawala wa Khilafah si mfumo usiojulikana ambao ulimwengu au watu wa India, hawaujui. India ilitawaliwa na mfumo huu wa utawala kwa karne nyingi ambao uliingiza India katika zama zake za dhahabu; kwani mfumo wa Kiislamu ulijenga usalama, amani, na ustawi kiasi kwamba India ilijulikana kama kapu la chakula la dunia. Hisa ya uzalishaji ya India ilikuwa zaidi ya 25% ya uzalishaji wa ulimwengu. Khilafah (kwa Kiarabu) ni mfumo wa Utawala wa Kiislamu uliowekwa na Mtume Muhammad (saw)

mwenyewe, kama taasisi ya utawala kuendelea baada ya zama za Mtume (saw) mjini Madinah ambako alikuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mkuu wa Dola. Katika taasisi hii Khalifa (kwa Kiarabu) ni mtu aliyechaguliwa kuongoza Serikali katika maeneo yote yanayotawaliwa na dola inayojumuisha ya Waislamu na Dhimmi (Wasio Waislamu). Khalifa ana mamlaka ya kuteua wasaidizi wake (katika kutawala), makadhi na pia wakuu wa idara mbalimbali za utawala au idara, ambazo pia anaweza kuziwakilisha. Khalifa pia huchukua chombo cha ushauri kilichochaguliwa kinachojulikana kama Shura (baraza la mashauriano). Huona kuwa ni jukumu jumla kuishi na kutekeleza Shariah katika maisha yao kwa Waislamu limekabidhiwa kwa pamoja kama amana kwa Khalifa na Waislamu katika kile kinachojulikana kama Bayah (ahadi ya utiifu). Khalifa anatarajiwa kutabikisha Shariah (sheria iliyomo ndani ya Quran na Hadith za Mtume). Shariah zinatawala mambo ya kibinafsi na ya umma. Masuala ya umma yanasimamia mambo ya utawala, uchumi, jamii na mahusiano ya kimataifa. Ama kuhusu mambo ya Kibinafsi hakuna kulazimishwa katika dini na ibada na kuhusu mambo ya kibinafsi yanayojumuisha ushiriki wa utawala, uchumi na jamii yanatawaliwa na mipaka ya Shariah.

Historia ya Khilafah: Ni ukweli uliothibitishwa wa historia kwamba taasisi ya Khilafah kama mfumo wa Utawala wa ulimwengu wa Kiislamu ilianza Madina baada ya zama za Mtume (saw) na kuendelea hadi 1924 ilipoondolewa rasmi na Mustafa Kemal Pasha huko Uturuki. Kwa kuzungumza kwa upana, baada ya Makhilifa 5 wa kwanza waliokuwa miongoni mwa maswahaba wa Mtume (saw), taasisi hiyo ilibakia mikononi mwa Bani Umayya (katika Syria ya leo), Abbasiyya (katika Iraq na Iran ya leo), na Uthmaniyya (katika Uturuki ya leo). Muendelezo wa Khilafah chini ya Khalifa mmoja ni kwa maelekezo ya moja kwa moja

ya Mtume (saw) katika Hadith (maneno yake); kwa kushindwa kufanya hivyo kulionekana kuwa ni dhambi kwa Waislamu. Kulikuwa na nyakati fupi katika historia ambapo umoja wa Khalifa ulibishaniwa na kusuluhishwa na vizazi vilivyofuata. Wakati wa upanuzi wa ukoloni wa dola za Ulaya kama matokeo ya mapinduzi ya Viwanda katika karne ya 19, baadhi ya maeneo ya Afrika na Asia yalitawaliwa na dola za kikoloni ingawa yalipingwa kote na Khilafah wakati huohuko Uturuki. WW1 vilishuhudia Khilafah ikiungana na Ujerumani mwaka 1914 kupigana dhidi ya Uingereza na Ufaransa na baada ya kushindwa, maeneo ya Khilafah yaligawanywa katika mamlaka mbalimbali ambazo baadaye zilikuja kuwa dola zilizoshindwa katika nchi zinazojulikana sasa kama nchi kubwa za Kiislamu katika Afrika Kaskazini, Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini. Asia hasa kwa kukusudia India, 1918 (baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia) hadi 1924 kilikuwa kipindi cha mashaka makubwa wakati suala la kuendelea kwa Khilafah lilikuwa ni wasiwasi mkubwa kwa Waislamu ulimwenguni kote pamoja na India. Hapo ndipo Harakati maarufu ya Khilafat ilipozinduliwa na viongozi wa Kiislamu kama vile ndugu Ali ambapo hata Wasiokuwa Waislamu waliunga mkono wito huo. Ilikuwa ni wakati huo ambapo Mahatma Gandhi aliandika katika 'Young India' mnamo Juni 1921 kuitetea Khilafah dhidi ya vikwazo vyote hata kama hakukuwa na Muslimaan (Waislamu) nchini India; kwa mtazamo wake kuhusu dori ya Khilafah katika kuondoa dhulma za kikoloni ilikuwa dhahiri sana. Vitabu kuhusu Khilafah na hukmu zake za Shariah vimeandikwa katika kipindi chote cha miaka 1400 kutoka duniani kote kwa lugha nyingi sana. Leo vinapatikana mara kwa mara katika maduka ya vitabu na mtandaoni. Hata hivyo, sheria ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, inayotaka kuendelea kwa mapambano kati ya haki na batili, iliwafanya watu wa batili kukosa dori ya Uislamu chini ya dola yake kwa karne nyingi za historia ya batili ambayo wanawafundisha watoto wao, licha ya kutambuliwa na watu wengi wenye fikra adilifu duniani kwamba wanadamu wote wana deni kwa Uislamu na Waislamu kwa mabadiliko angavu waliyoyaleta katika maisha ya watu.

Kuhusu Hizb-ut-Tahrir: Hizb-ut-Tahrir (Chama cha Ukombozi) ni chama cha kisiasa kilichoanzishwa mwaka wa 1953 na mwanachuoni mkubwa, mwanafikra wa kisiasa na kadhi Sheikh Taqiuddin Nabhani. Hizb inafanya kazi ya kujenga rai jumla katika nchi za Kiislamu kupendelea mfumo wa utawala wa Kiislamu, Khilafah, kwa kuiga mfano wa Mtume (saw). Hii inahusisha kuwasilisha masuluhisho ya Kiislamu ili kushughulikia matatizo ya kisasa, harakati za kisiasa na hatimaye kufanya kazi kwa ajili ya mabadiliko ya kisiasa katika nchi za Kiislamu kwa njia isiyo ya vurugu. Katika nchi zisizo kubwa za Kiislamu, hizb inahimiza jamii ya Waislamu kuwa watetezi wa Uislamu na kulinda kitambulisho chake cha Kiislamu. Uanaharakati ni pamoja na kusoma masuluhisho ya Kiislamu ya matatizo ya kisasa ya kiuchumi, kijamii na kiutawala kwa upande wa Shariah, kutoa wito kwa makundi yote ya watu dhidi ya dhulma

za kipote cha watawala, ambao wengi wao wanafurahia ufadhili wa dola za kikoloni kwa nia ya kukandamiza aina yoyote ya mwamko wa kisiasa katika ulimwengu wa Kiislamu. Uanaharakati duniani kote unajifunga na njia za kifikra kama wajibu wa Sharia kuhusiana na njia ya mwamko wa watu. Aina yoyote ya ghasia za watu binafsi au makundi kwa ajili ya mabadiliko ya kisiasa inaonekana kama ukiukaji wa njia ya mwamko wa watu. Hizb imechapisha rasimu ya katiba inayozingatia kanuni za Shariah na kuifanya ipatikane kama pendekezo kwa Khilafah ijayo. Rai na mitazamo ya hizb iko hadharani kikamilifu, mradi tu nchi hazizuii tovuti au wachapishaji, na hakuna rai, maoni au vitendo tofauti vya hizb na yale yaliyosemwa hadharani. Hizb inaweka hili kuwa sharti kwa wafuasi wake, kufanya kazi na hizb. Leo hizb ipo katika zaidi ya nchi 40 zikiwemo baadhi za nje ya ulimwengu wa Kiislamu; na tangu kuanzishwa kwake, haijakengeuka katika njia yake.

Enyi Watu! Hizb ut Tahrir ni mchungaji (kiongozi) asiyelidanganya kundi lake (watu), na lengo lake imedhamiria kuwaokoa wanadamu kutokana na utumwa wa ubepari na kuporomoka kwa maadili yake hadi kwenye uadilifu wa Uislamu ambao kamwe hauwadhulumu, na inafanya kazi hii adhimu bila malipo yoyote kutoka kwa watu, kwa kufuata mfano wa manabii na mitume; wanaoongozwa na bwana wa viumbe, Muhammad, rehema na amani zimshukie. Hizb ut Tahrir haiogopi dhulma ya madhalimu, na haiogopi lawama ya mwenye kulaumu, na inajua kwamba dola za Magharibi na vibaraka wao duniani wanafanya kazi kwa bidii ili kuwazuia watu kutafuta njia badali ya kihadhara ambayo itawaokoa kutoka kwenye makuha ya ulafi, machafuko na ubaguzi wa rangi wa kiskela. Kwa hiyo nguvu hizi ovu zinaficha ukweli wa Uislamu na ukweli wa Hizb ut Tahrir inayobeba Uislamu huu. Bali wanaipotosha sura yake ili watu waliodhulumiwa wasiongozwe kwenye yale ambayo yamo mikononi mwa kundi la kheri kubwa, na yanayobebwa na Hizb ut Tahrir ni njia badali ya kihadhara inayowaokoa watu kutokana na majanga waliyomo ndani yake yaliyosababishwa na tawala za kibinadamu. Kwa hivyo ni wajibu kwa kila mwokozi mwaminifu na asiye na upendeleo, awe Muislamu au asiye Muislamu, mwanamume au mwanamke, msomi au aalim, mwana usalama au mwanasheria, mhadhiri au profesa, kufanya kazi kwa bidii ili kuutabanni Uislamu mtukufu kama mfumo kamili wa maisha. Mwenyezi Mungu (swt) asema katika Kitabu chake,

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ

“Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya Haki ipate kushinda dini zote, ijapo kuwa washirikina watachukia.” [9:33].

H. 15 Dhu al-Hijjah 1444

Hizb-ut-Tahrir

M. : Jumapili, 25 Juni 2023

Afisi Kuu ya Habari

Matatizo ya Kimetaboliki

Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

Ali Nassoro Abu Taqiuddin
Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir



Ni muhimu kuweza kuelezea nini metaboli, ili kuweza kupata ufahamu msingi kuhusu kichwa. *Metaboli (metaboliki)* ni mchakato wa kikemikali ambao mwili unabadilisha chakula kuwa nishati. Mchakato huu hujumuisha kukivunjavunja chakula kuwa sukari na asidi kupitia nidhamu ya kumeng'anya. Nishati inaweza kutumika papo kwa papo au kuhifadhiwa katika viungo vya mwili kama vile ini na mishipa. Hivyo basi, mchakato wa kimetaboliki hufanyika kwa mpangilio wa hali ya juu na lau utakengeuka basi unaweza kupelekea kuwoko kwa masula tofauti ya kiafya.

Sasa, matatizo ya kimetaboliki pia hujulikana kama matatizo ya uasi wa insulini. Ni mjumuiko wa hali ambazo huzidisha hatari ya kupata unene wa kupita kiasi, kisukari, magonjwa ya mishipa ya moyo, shinikizo la damu na matatizo mengine makubwa ya kiafya. Yana sababishwa kimakusudi na kutojifunga na miko ya nguzo nne za afya bora, ambazo ni **lishe bora, mazoezi, kufunga, na kulala.**

Takwimu za kimataifa ztoa taswira ya kutamausha ya hali mbaya ya kiafya ya kijamii. Hivi sasa, tuna watu zaidi ya milioni 870 ambao hawana lishe bora, bilioni 1.745 wana uzito kupita kiasi na milioni 837 wanakaribia kutumbukia katika kisukari. [Worldometers.info, 17 Juni, 2023]. Gharama ya kimataifa ya kiafya ya kisukari ni dola bilioni 375 kwa mwaka. Na ile ya uzito wa kupita kiasi ni dola trilioni 2. [Matthew Walker, PhD, *Why We Sleep*

(2017), uk. 169]. Tumo katika janga hili la kiafya kama natija ya kukataa kwetu kujifunza upya yale yaliyomo ndani ya akili zetu kuhusiana na nini maana ya afya bora. Kwa maana nyingine, sisi ni watumwa wa mazoea yetu na hivyo kutupelekea kuwa wahanga wa maamuzi mabaya tuliyochukua ili nasi tuweze kwenda na mkumbo wa kijamii. Au kimakusudi kutofanyiakazi ukweli kwa kuogopa jamii itatutenga au mihemko yake.

Kwa kifupi wacha tueleze umuhimu wa kujifunga na misingi minne ya afya bora. **Kwanza, lishe:** wala chakula cha kweli; nikimaanisha ambacho hakisababishi matatizo? Najua utajibu NDIO. Lakini, subiri kwanza kwa muda mfupi, unaweza kutafakari upya tena jibu lako. Fauka ya hayo, unaweza kuwa na shaka na piramidi ya chakula ambayo umefunzwa na kuikubali kuwa eti ndio msingi wako wa lishe bora. Ilhali sio chochote bali ni ujanja wa utafutaji soko kwa njia ya kutumia afya, badala yake inakufanya kuwa mgonjwa huku makampuni makubwa ya kutengeneza dawa na bidhaa za vyakula zikitia faida.

Kwa lugha nyepesi virutubisho vimegawanyika mara mbili; virutubisho muhimu (protini) na virutubisho visivyo muhimu (kabohaidrati). Tofauti baina yao ni kwamba virutubisho muhimu vinahitajika kuliwa kupitia lishe ilhali virutubisho visivyo muhimu miili yetu inaweza kuvitengeneza vya kutosha kindani. Ili kuelezea, tutatoa mifano ya vyakula aina mbili ambavyo ni kabohaidrati

Endelea... UK 8

(sukari) na protini (nyama); na metaboli ya vyakula hivyo itatupa taswira ya ima tunakula vyakula vya kweli (virutubisho muhimu) au la.

Metaboli ya kabohaidrati (sukari) ni kama ifuatavyo; ndani ya mdomo wako inavunjwa na kuwa glukosi na fruktosi. Ndani ya kongosho tunayo homoni ya insulini, ambayo kazi yake msingi kushusha sukari katika damu. Insulini huzichochea seli za mwili kufyonza glukosi kutoka katika mkondo wa damu. Upande mwingine, fruktosi ina metaboliwa na ini kuwa glukosi, laktosi na glaikogeni. Ini linaweza kutumia na kuhifadhi kiwango cha fruktosi kama glaikogeni kwa wakati mmoja. Viwango stahiki vya glaikogeni vinapokuwa vimejaa, fruktosi hubadilishwa na kuwa mafuta ya ini kupitia njia ya inayojulikana kama de novo lipogenesis.

Kabla hatujaelezea metaboli ya protini (nyama), ni muhimu kutambua kwamba: 'protini inacheza dori kubwa katika uhai. Ndani ya seli, protini ndio zenye kufanya kazi ngumu. Lau DNA ndio Afisa Mkuu msimamizi, basi protini ndio majeshi ya wafanyakazi wa mkono wanao hakikisha biashara inakwenda vizuri. Protini inatoa muundo, inajenga mishipa na inaboresha michakato ya kimetaboliki. Ndio zinazotumika kama viunganishi, homoni na kubeba taarifa, kusambaza jumbe kutoka nje ya seli na kurudi kwa DNA – zikiashiria ni jeni zipi zifanye na zipi zisifanye kazi. DNA hupeana kodi ya kutengeneza protini za seli – ujumbe uliomo ndani ya kila jeni hutafsiriwa na kuwa kitendo na protini. Jeni moja ni sawa na protini moja.' [Travis Christofferson, *Ketones the Fourth Fuel* (2020), uk. 38].

Sasa, metaboli ya protini (nyama); ndani ya tumbo lako huvunjwa na kuwa amino asidi. Amino asidi hutumika kutengeneza protini. Lau amino asidi zitakuwepo kwa kuzidi, mwili hauna uwezo au mpangilio wa kuzihifadhi; hivyo basi, hubadilishwa na kuwa ketoni au zikaozeshwa.

Kwa kifupi, milo ambayo ina wingi wa kabohaidrati hususan zama hizi za bidhaa za vyakula vya kusindika, inaleta mzunguko hatari kwa afya zetu. Kwa kuwa kila unapokula kabohaidrati (sukari): glukosi hupanda na insulini nayo huitikia mpaka pale itakapokuwa imeasi, na kuzidi kwa uhifadhi wa mafuta katika ini na mishipa. Kwa sababu hiyo inapelekea sintofahamu katika mpangilio wa homoni muhimu kama vile leptini na ghrelini. Leptini hutumika kuchochea hisia ya kujihisi kushiba. Ghrelini hutumika kuchochea hisia ya kiwango cha juu cha kuhisi njaa. Kwa kuongezea, huharibu hadi hisia zetu za kuonja.

Pili, mazoezi: umefanya mazoezi leo? Mazoezi, pia hujulikana kama shughuli za kimwili, ni aina yoyote ya harakati ambayo inaushughulisha mwili kwa kiwango kikubwa tofauti na kawaida ya kiwango cha kila siku. Kufanya mazoezi ni muhimu kutokana na sababu zifuatazo kuu: moja – inaboresha muitiko wa insulini katika mishipa ya mifupa. Pili – hupunguza msongo wa

mawazo, kutokana na natija ya kutolewa kotisoli. Tatu – hufanya mzunguko wa TCA (tricarboxylic acid) kuwa na kasi, kuiondoa sumu ya fruktosi, kuboresha muitikio wa insulini katika ubongo. Jitahidi iwezekanavyo kujiepusha kukaa tu. Kukaa tu inamaanisha kuketi kwa muda mwingi au inaashiria mtu au kazi ambayo isiyo ushughulisha mwili. Zipo aina nyingi za mazoezi lakini jikite katika yale ambayo ni muhimu zaidi: kutembea mwendo kasi, chumba cha mazoezi (kufanya mazoezi ambayo yatashughulisha kundi la mishipa kwa wakati mmoja: kunyanyua uzani ukiwa umelala (bench press), ukiwa umechuchumaa (squats), ukiwa umesimama na kuinama (dead lift), ukiwa umeinama (row), kushika na kujivuta juu (pull-ups) au mazoezi ya kasi mno ya kujirudiarudia mpaka utakapochoka (HIIT) kama (jogging, push-ups) nk.

Tatu, kufunga: umefunga leo? Kufunga kinyume chake ni kukaa njaa. Kufunga ni kutia nia kujiepusha kutokula na kunywa kwa muda fulani. Zipo sababu nyingi za kufunga, lakini lengo la muktadha wetu ni metaboliki. Katika zama hizi za bidhaa za vyakula vya haraka vilivyo sindikwa ambavyo vinatufanya tutake kula zaidi na zaidi. Kwa kuongezea, vinatusababishia kuwa na uzito wa kupita kiasi tukikaribia kutumbukia katika shimo la kisukari.

Kufunga lazima tukujumuishe katika mkakati wetu wa lishe bora ndani ya maisha yetu ya kila siku. Kudhibiti kula na /au kunywa kwa muda maalumu kila siku. Kwa mfano, tule chakula mara moja kwa siku baina ya saa sita na saa nane mchana au baina ya jioni saa kumi na moja na usiku saa moja (saa mbili pekee). Haitotusaidia tu kupunguza uzani, bali itatutua changamoto nyingine nyingi za kiafya. Tunapofunga hupelekea miili yetu kuingia katika ketosisi. Ketosisi ni hali ya kimetaboliki ambapo mwili huhoma mafuta yaliyo hifadhiwa. Kufunga kwa muda mrefu, kama saa 48 / 72 kwa kunywa maji inapendekezwa, kwani mwili huingia katika hali ya autofaji (autophagy). Autofaji ni hali ya kimaumbile ya mwili, katika mchakato wa kujihifadhi wenyewe kwa kuzitoa seli au sehemu za seli ambazo zimeharibika au hazifanyikazi tena kupelekea kuzitibu na kuufanya upya mpangilio wa seli.

Nne, usingizi: umepata usingizi mwanana? 'Wanadamu hawalali namna mpangilio ulivyowekwa. Idadi ya vipindi vya kulala, muda wa usingizi, na wakati ambapo usingizi hupatikana yote yamebadilishwa juu chini kutokana na usasa.

Katika mataifa yote yaliyoendelea, watu wazima wengi hivi sasa wanalala kipindi kimoja – kwa maana tunalala kipindi kimoja kirefu usiku, ambacho muda wa wastani wake hivi sasa ni chini ya saa saba. Zuru tamaduni ambazo bado hazijaathiriwa na umeme na utaona aghalabu mambo tofauti. Makabila ya wawindaji – wakusanyaji kama vile Wagabra nchini kaskazini mwa Kenya au watu Wasan katika Jangwa la Kalahari,

Endelea... UK 9

ambao maisha yao hayajabadilika vile zaidi ya miaka elfu, wanalala vipindi viwili. Makundi yote haya mawili wanapata usingizi mrefu kipindi cha usiku (saa sabab hadi nane, wakifaulu takribani saa saba za usingizi), wakifuatiwa na dakika thelathini – sitini za mapumziko mchana.

Na pia upo ushahidi wa kuchanganyika kwa vipindi vya kulala, vinavyo athiriwa na muda wa mwaka. Makabila kabla zama za viwanda, kama vile Wahadza nchini kaskazini mwa Tanzania au Wasan wa nchi ya Namibia, hulala vipindi viwili miezi ya joto, wakijumuisha na dakika thelathini – arubaini za mapumziko mchana wa juu. Kisha wakibadilisha kwa kiasi kikubwa kuwa kipindi kimoja wakati wa miezi ya baridi. [Matthew Walker, PhD, *Why We Sleep* (2017), p. 67].

Usingizi ni nguzo muhimu katika kupata afya bora. Vitendo vyovyote ambavyo vinapelekea kughairisha na kunyima usingizi hupelekea kuwa na matokeo hatari ya kiafya katika hali ya muda mfupi na mrefu. Mfano wa janga kubwa ni lile la muendeshaji gari kisha akalala au akafunga macho kwa sekunde kadhaa (microsleep) katika barabara iliyo na shughuli nyingi au barabara kuu. Mfano mwingine ni ule wa mtoto mdogo ambaye amenyimwa usingizi na wazazi wake eti kwa jina la elimu. Jambo moja lazima liwe wazi, madeni ya usingizi hayalipiki! Usingizi ndio nguzo inayodharauliwa zaidi miongoni mwa hizi nne, lakini ndio ambayo nguzo nyingine tatu zilizobakia zinaizunguka hiyo, kwani mwili unahitaji usingizi kuweza kufanyakazi kwa kiwango stahiki.

Kwa kuhitimisha, matatizo ya kimetaboliki lazima yatatuliwe kwa ngazi ya kibinafsi kwa kujaribu kujumuisha lishe bora iliyo na wingi wa protini, mazoezi ya mara kwa mara, kufunga kwa muda kutokula lakini unywe maji na pia kupata lepe la usingizi mchana na kulala mapema linapokuchwa jua. Kwa kuongezea, sera zitabuniwa na dola ya Kiislamu ya Khilafah itakayosimama hivi karibu kwa njia ya Utume. Sera ambazo zitadhamini afya na mazingira salama kwa raia. Khilafah itapiga marufuku makampuni yanayotia faida kupitia watu kupata dhiki. Kujifunga na Shari'ah ya Kiislamu na wala sio faida, itakuwa ndio kipimo cha kuhifadhi afya za raia. Kampeni za kiafya zitafanywa ili kuhakikisha kuwa raia wanakula lishe bora, wanafanya mazoezi, wanafunga na kupata usingizi mwanana miongoni mwa masuala ya kidharura ya kiafya na yenye kipaumbele. Kwa sababu raia walio na afya ndio dola iliyo makinika. Raia wenye afya wana dori kubwa kwa Khilafah kuwa mshika hatamu wa kimataifa.



Kafara ya Kuvunja Kiapo (Kafarat ul-Yameen)

01 Dhul Hijjah 1444 H - 19/06/2023 M

Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah

Swali:

Assalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Sheikh wetu muheshimiwa,

Je, kafara ya kuvunja kiapo (kafarat ul-yameen) inaweza kupewa mtoto mchanga ambaye hali chakula anakunywa tu maziwa ya mama pekee au maziwa ya unga ya watoto wachanga? Iwapo kafara imetolewa na mtu akasahau kuhusu hali hii (imepewa mtoto mchanga), je mtu huyo anapaswa kurudia kutoa kafara kwa masikini?

Na swali jengine linalohusiana na kafara ya kuvunja kiapo: Je, inatosha kumlisha masikini mara moja, au ni lazima kumlisha mara mbili (chakula cha mchana na jioni?)

Na swali la tatu: mtu anayeishi barani Ulaya na akatoa kafara ya kiapo kwa maskini nchini Ukraine kwa kufuata kiasi cha kafara ya kiapo nchini Ukraine. Je, ilikuwa ni lazima kwake kufuata kiasi cha kafara barani Ulaya, au ilitosha kufuata kiasi katika nchi iliyotumwa?

Jibu:

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

1- Kanuni msingi kuhusiana na kafara ya kiapo (kafarat ul yameen) ni maneno ya Mwenyezi Mungu (swt):

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا عَقَّدْتُمُ الْأَيْمَانَ فَكَفَّارَتُهُ إِطْعَامُ عَشْرَةِ مَسَاكِينَ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعَمُونَ أَوْ كِسْوَتُهُمْ أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ ذَلِكَ كَفَّارَةُ أَيْمَانِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ وَاحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“Mwenyezi Mungu hatakushikeni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini atakushikeni kwa mnavyo apa kweli kweli kwa makusudio. Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnacho walisha ahali zenu, au kuwavisha, au kumkomboa mtumwa. Asiye pata hayo, basi afunge siku tatu. Hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapo apa. Na hifadhini yamini zenu. Namna hivyo Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake ili mpate kushukuru.” [Al-Ma'idah: 89]. Kuwalisha masikini kumi ni mojawapo ya machaguo yaliyotajwa katika ayah hii:

“Basi kafara Endelea... UK 11

yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnacho walisha ahali zenu” [Al-Ma'idah: 89].

2- Inaeleweka kutokana na aya hiyo tukufu kwamba idadi ya kumi ni ya kulazimisha, yaani, masikini kumi lazima walishwe, hivyo sio sahihi kulisha maskini mmoja mara kumi, kwa mfano. Tumefafanua hili hapo awali katika Jibu la Swali la tarehe 29/4/2022 M, ambapo yafuatayo yalielezwa:

[na rai ambayo naoina kuwa sahihi zaidi ni kwamba ikiwa maandiko yametajwa na idadi fulani ya watu masikini, kama vile

فَكَفَّارَتُهُ إِطْعَامُ عَشْرَةِ مَسَاكِينَ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعَمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْوَتُهُمْ
“**Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnacho walisha ahali zenu au kuwavisha**” [Al-Ma'ida: 89]

أَيُّهَا...**Na asiye weza hayo basi awalishe masikini sitini.**” [Al-Mujadila: 4]. Katika hali hii, idadi iliyotajwa hapo juu (kumi, sita) ni lazima izingatiwe, iwe utoaji ni wa aina au wa thamani, kwa sababu nambari ndio iliyo dhamiriwa, ni ufungaji wa lazima, lakini ikiwa andiko linahitaji kuwapa masikini pasi na kutaja idadi, inaruhusiwa kumpa masikini mmoja kwa sababu hakuna ufungaji wa idadi, na pia yaweza kupeanwa kwa zaidi ya masikini mmoja, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu (swt) kuhusiana na zaka:

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسْكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمَوْلَّاتِ فُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ
وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

“**Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanao zitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni waajibu ulio faridhiwa na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.**”

[At-Tawba: 60]. Kwa hivyo inajuzu kwa mwenye kutoa Zaka kumpa masikini mmoja, na inajuzu kuigawanya kwa masikini wengi, kwa sababu hakuna idadi maalum katika Aya, bali neno "masikini" limetajwa namna hiyo bila ya idadi... Lakini anazingatia tu kwamba wanastahiki kupewa zaka kwa sababu wamesifiwa kuwa ni masikini.]

3- Kwa hiyo, kukamilika kwa kafara kunahitaji kuwalisha masikini kumi chakula cha wastani, na hii ina maana kwamba masikini anayepewa kafara ndiye anayeweza kula chakula cha wastani. Ama mtoto anayenyonyesha sidhani kuwa amejumuishwa katika fahamu hii, na kwa hivyo hahesabiwi miongoni mwa masikini wanaolishwa katika kafara ya kiapo. Ikiwa mtu alisimama na kupeleka chakula kwa familia maskini yenye watu kumi, akiwemo mtoto mchanga, basi kafara hii haijakamilika; ni sawa na kulisha watu tisa na sio kumi, kwa sababu mtoto hawi chini ya fahamu ya wale wanaolishwa. Hii ndiyo ninayoiona kuwa sahihi zaidi na ndiyo ninayoridhika nayo. Kwa hiyo, ni lazima akamilishe kwa kumlisha

masikini mwingine pamoja na wale aliowalisha ili kukamilisha kafara ya masikini kumi. Hii ni tofauti na mtoto anayekula chakula, kama vile mvulana mwenye akili razini na mfano wake, kwani hawa wanahesabiwa katika kafara. Ikiwa katika familia masikini walikuwepo watoto kama hawa, basi kafara ni halali kwa kuwalisha, kwa sababu wanaingia katika fahamu ya wale wanaolishwa.

4- Mafakih wamekhitilafiana katika kupambanua kiasi cha chakula kwa kila masikini katika kafara ya kuvunja kiapo (kafarat ul yameen), na katika aina ya chakula kinachotolewa kafara n.k. Encyclopedia ya Fiqh ya Kuwait

[“Pili: Kuhusu kiasi”

- Maliki, Shafi'i na Hanbali wana rai kwamba ni sharti kwamba kila masikini apewe kibaba (mudd) moja (kipimo cha uzito) kutoka katika sehemu ya chakula cha nchi kinacholiwa zaidi, na hairuhusiwi kutoa thamani ya chakula kulingana na andiko la aya:

فَكَفَّارَتُهُ إِطْعَامُ عَشْرَةِ مَسَاكِينَ
“**Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi**” [Al-Ma'idah: 89]. Ni sharti kwamba hisa zisipunguzwe, kwa hivyo haijuzu kuwapa masikini ishirini vibaba (mudd) kumi; kwa kila mmoja wao nusu kibaba isipokuwa atimize kwa kumi hao kile kilichopungua. Vile vile inatajikana ulishaji uwe kwa watu kumi, kwa hivyo uzushi haufai, hivyo ikiwa alilisha watano na akavisha tano, haijuzu. Vile vile inatakiwa kibaba kitolewe kwa kila mmoja katika watu kumi kwa msingi wa umiliki, na hairuhusiwi kwa mujibu wa madh'hab ya Malik kurudia kumpa mmoja. Mahanafi wana rai kwamba ni sharti kwamba kila masikini apewe nusu pishi (saa') (kipimo cha uzito) ya ngano, au pishi ya tende au mawe, au thamani ya hizo kwa pesa au ofa biashara, kwa sababu lengo ni kulipa hitaji, na hilo linaweza kufikiwa kwa thamani.

Ama kiasi cha chakula kinachoruhusiwa kwao: milo miwili yenye shibe, yaani, inatakiwa kila masikini apate chakula cha mchana na cha jioni, na vivyo hivyo akiwapa chakula cha jioni na suhur, au awape chakula cha mchana mara mbili na kadhalika, kwa sababu ni milo miwili iliyokusudiwa.

Lakini akimpa mtu mmoja chakula cha mchana na mwingine chakula cha jioni moja, hiyo si halali, kwa sababu atakuwa amegawanya chakula cha wale kumi kuwa ishirini, jambo ambalo si sahihi.

Vile vile wameweka sharti kwamba asitoe kafara yote kwa masikini mmoja kwa siku moja mara moja au tofauti kwa zaidi ya mara kumi. Lakini ikiwa alimlisha masikini mmoja kwa siku kumi, chakula cha mchana na cha jioni, au akampa masikini mmoja siku kumi kila siku nusu pishi, hiyo inajuzu kwa sababu hitaji linafanywa upya kila siku na kumfanya mithili ya masikini mwengine, kana kwamba

Endelea... UK 12

alitumia thamani hiyo kwa watu kumi maskini.

"Tatu: Kuhusu aina"

- Hanafi wana rai kwamba kinachotosheleza katika kulisha ni ngano, au mawele, au tende, unga wa kila moja ya hizo ni mithili ya asili yake kwa kipimo, yaani, nusu pishi katika unga wa ngano na pishi katika unga wa mawele na ikasemwa: Kinachozingatiwa katika unga ni thamani, sio kipimo, na inajuzu kuvua thamani kutoka kwa aina zisizokuwa hizi. Maliki walikwenda kwenye ukweli kwamba kulisha ni kutokana na ngano ikiwa wameila, kwa hivyo haikubaliki kutoka kwa mawele au mahindi au nafaka nyinginezo. Ikiwa walikula isiyokuwa ngano, basi kilicho sawa nayo ni kushiba, na sio kipimo (kinachotolewa). Shafii wana rai kwamba kulisha ni kutokana na nafaka na matunda ambayo zakat inastahili kutolewa, kwa sababu miili huimarishwa nazo, na inatakiwa iwe kutoka kwa wingi wa chakula cha nchi. Hanbali walikwenda kuweka sharti kwamba kulisha kunapaswa kuwe kutokana na ngano, mawele na unga wao, tende na zabibu kavu, na hakuna kitu chengine chochote kinachoruhusiwa, hata kama ni chakula cha nchi yake, isipokuwa kiwa vyakula hivyo havipatikani.]

Mwisho.

5- Ninachokiona kuwa sahihi zaidi kuhusiana na kulisha masikini kumi ni kwamba wanapewa milo miwili ili iwe maana ya kweli ya Aya:

فَكَفَّارَتُهُ إِطْعَامُ عَشْرَةِ مَسَاكِينَ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعَمُونَ أَهْلِيكُمْ

“Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnacho walisha ahali zenu”

[Al-Ma'idah: 89]. Kulisha familia ni mara mbili kwa siku, ili iweze kuitwa kulisha, kama vile chakula cha mchana na chakula cha jioni; Vyenginevyo, hajamaliza kulisha familia yake, na vile vile kuhusu masikini katika kafara, ni lazima awalishe mara mbili kwa siku mpaka kafara ikamilike, basi akitosheleza kwa chakula cha mchana bila chakula cha jioni, au kwa chakula cha jioni bila chakula cha mchana hii haikubaliki, na pia, Shariah imekifanya chakula katika Ramadhan kuwa milo miwili: chakula cha kabla ya alfajiri na cha futari, hivyo kulisha kamili ni kwavyo au mfano wake.

6- Ama kuhusu swali lako: (mtu anayeishi Ulaya na akatoa kafara ya kiapo kwa masikini wa Ukraine kwa kufuata kiasi cha kafara ya kiapo cha Ukraine. Je, ilikuwa ni lazima kwake kufuata kiasi cha kafara huko Ulaya, au ilitosha kufuata kiasi katika nchi ilikopelekwa?) jibu la hilo na kile nilicho na imini nacho ni kwamba kiasi kinachotumwa ni kulingana na wastani wa chakula katika nchi ambayo mtu anayepewa kafara inaishi, na hiyo ni kwa sababu Aya tukufu inasema:

[فَكَفَّارَتُهُ إِطْعَامُ عَشْرَةِ مَسَاكِينَ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعَمُونَ أَهْلِيكُمْ]

“Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa

chakula cha wastani mnacho walisha ahali zenu”

[Al-Ma'idah: 89]. Hili humfanya ahisi kuwa kulisha ni kulingana na mahali alipo mtu huyo, kwa sababu kinachotakiwa ni kuwalisha masikini kumi kutokana na wastani wa kile anacholisha familia yake. Ikiwa alilisha, kwa mfano, nchini Ukraine kwa dolari kumi, basi hizi zinaweza kutosha kulisha watu kumi masikini huko, lakini hazitoshi kulisha watu kumi masikini kulingana na hali ya Ulaya. Kwa mfano, anapaswa kulisha kwa dolari mia moja ili aweze kulisha kwa wastani wa kile anacholisha familia yake. Kwa hivyo, nadhani ni bora na busara zaidi kutoa kiasi cha kulisha watu kumi maskini katika nchi anayoishi.

Hili ndilo ninaloliona kuwa sahihi zaidi, na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi, ni Mwenye hekima.

Ndugu Yenu,

Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah